East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature
OPEN ACCESS
*Abbreviated Key Title: East African Scholars J Edu Humanit Lit*
ISSN: 2617-443X (Print) & ISSN: 2617-7250 (Online)
Published By East African Scholars Publisher, Kenya
Volume-5 | Issue-10 | Oct- 2022 | DOI: 10.36349/easjehl.2022.v05i10.001

**Original Research Article**

# Upambanuzi wa Miundo ya Toponemia katika Jamii: Mfano kutoka Jimbo Dogo la Maara nchini Kenya

David Micheni Mutegi[1], Dr. Allan Mugambi[2], Dr. Timothy Kinoti M'Ngaruthi[3*]
[1]Tharaka University, P. O. Box 193 Marimanti, Kenya
[2]Chuka University, P. O. Box 109 Chuka, Kenya
[3]University of Embu, P. O Box 6 Embu, Kenya

**Article History**
**Received:** 21.08.2022
**Accepted:** 24.09.2022
**Published**: 02.10.2022

**Journal homepage:**
https://www.easpublisher.com

**Quick Response Code**

**Abstract:** Makala hii imewasilisha uchunguzi uliofanywa kuhusu michakato na mbinu zilizotumika katika uundaji wa toponemia katika jamii. Lengo mahsusi la utafiti huu lilikuwa kupambanua miundo ya toponemia katika eneo la Mwimbi na Muthambi jimboni dogo la Maara. Maeneo haya yaliteuliwa kwa vile yalihusiana kilugha na kiutamaduni hasa katika suala la onomastiki. Nadharia ya Ujinaishaji ndiyo ilitumiwa kuongoza utafiti huu. Data ya utafiti huu ilikusanywa kwa kupitia kwa ya mahojiano ya ana kwa ana pamoja na hojaji. Mahojiano yalimwezesha mtafiti kupata data ya kutosha na halisi moja kwa moja kutoka kwa wahojiwa. Hojaji ilimwezesha mtafiti kukusanya data kwa urahisi katika maeneo mengi na kutoka kwa sampuli kubwa. Walengwa katika utafiti huu walikuwa wakaazi wa Mwimbi na Muthambi. Usampulishaji ulifanywa kimaksudi kwa kuhusisha machifu 5 wa kata 5 za Mwimbi na Muthambi na manaibu wa chifu 25 kutoka kata ndogo 25 za eneo hili. Watawala hao walichaguliwa kwa sababu wao ni wenyeji wa eneo hili walio na habari kuhusu maeneo yao ya utawala, na hivyo wangetoa habari kamilifu kuhusu maswali ya utafiti. Sampuli nyingine ya Wazee 20 wenye umri wa miaka sabini na zaidi walichaguliwa kimakusudi kwa kutumia mbinu ya kimtandao ili kutoa habari kuhusu michakato ya uundaji wa toponemia za shule za msingi katika eneo la Mwimbi na Muthambi. Sampuli ya wazee iliweza kupatikana kwa urahisi kwa sababu ndio wanaopata pesa za wazee na walijulikana katika vijiji vyao. Uchambuzi na uwasilishaji wa data ya utafiti huu ulitumia mkabala wa kimaelezo kulingana na madhumuni na swali la utafiti. Matokeo ya utafiti huu ni marejeleo muhimu kwa watafiti wengine watakaoshughulikia vipengele vya onomastiki katika lahaja ya Kimwimbi na Muthambi. Aidha, utafiti huu ulibainisha michakato mbalimbali ya uundaji wa toponemia katika jamii.

**Keywords:** Anthroponemia, Onomastiki, Toponemia, Uundaji; Upambanuzi.

**Copyright © 2022 The Author(s):** This is an open-access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution **4.0 International License (CC BY-NC 4.0)** which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium for non-commercial use provided the original author and source are credited.

## UTANGULIZI

Toponemia ni amali muhimu kwa maisha ya kila siku na maendeleo ya watu. Humwezesha mtu kutekeleza majukumu na wajibu wake wa kila siku katika nyanja mbalimbali za kiutamaduni, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Wanaisimu mbalimbali wamechunguza mbinu zilizotumiwa katika kuunda majina ya mahali katika sehemu mbalimbali. Matinde (2012) alifafanua mbinu ya uradidi iliyotumiwa katika uundaji wa majina ya mahali. Alisema kuwa uradidi ungeweza kuwa wa nusu ambapo sehemu tu ya neno hurudiwa au uradidi kamili ambapo jina zima hurudiwa ili kuunda jina mpya. Muundo kama huu ulitumiwa kuunda majina ya mitaa ya kisiwani pemba kama vile mtaa wa *chakechake* ambapo neno *chake* ndilo limekaririwa. Matinde (keshatajwa) alieleza mbinu ya akronimu inayomaanisha ufupishaji ambayo hutokana na kitenzi "fupisha" kilicho na maana ya kufanya kitu kuwa kifupi au kupunguza urefu. Mbinu hii huhusisha kuondoa baadhi ya vipashio au silabi na kuacha sehemu tu ya neno asilia. Rubanza (1996) alifafanua mbinu ya uhulutishaji ambapo vijisehemu vya maneno huwekwa pamoja ili kuunda neno mpya. Kwa mfano ametoa jina *Chanjawiri* kutokana na jina *Chanjaa la Mjawiri* ambapo vijisehemu vya maneno vilitumiwa kuunda jina *Chanjamjawiri.* Aidha, Matinde (keshatajwa) aliongeza mbinu ya utohoji inayotumiwa kuunda majina kwa kufanya marekebisho ya kifonolojia na mofolojia katika jina la lugha nyingine. Plag (2003) anasema kuwa lugha hutofautiana katika mifanyiko ya kimofolojia katika kuunda maneno yake. Bauer (1993) anajadili zaidi ya michakato sita inayotumika katika uundaji wa maneno ya Kiingereza na kudai kuwa mabadiliko ndiyo hutumiwa sana kwa vile hakuna vikwazo vya kifonolojia. Bauer (keshatajwa) anaongeza kwamba kuna majina mengi ya Kiingereza yaliyoundwa kwa kutumia mbinu ya mwambatano kama vile nomino na nomino. Halle (1973) alidai kuwa majina yote katika

***Corresponding Author:** Dr. Timothy Kinoti M'Ngaruthi
University of Embu, P. O Box 6 Embu, Kenya

lugha hayawezi kutolewa kwa kutumia kanuni za kawaida na za jumla kwa hivyo kuna njia nyingine za kutoa majina katika lugha. Kwa upande wake Mphande, (2006), mchakato wa kimofolojia ulio wazi na unaotumika sana katika uundaji wa majina ni uambishaji awali au tamati. Jensen na Jensen (1990) wanasema kuwa mchakato wa mabadiliko hutokea katika lugha ya Kiingereza na Kifaransa ambapo kando na mchakato wa uambishaji kuna michakato mingine kama vile uchangamano na mabadiliko. Jensen na Jensen (keshatajwa) wanaeleza kuwa mchakato fulani unaweza kuelezwa vyema katika lugha fulani na kutofafanuliwa katika lugha nyingine kwa mfano uchopekazi ulio wazi katika Kiingereza. Haspelmath (2002) anaeleza kuwa jambo linaloweza kuelezwa kimofolojia katika lugha fulani huweza kuelezwa kwa neno tofauti katika lugha nyingine au likakosa kuelezwa katika lugha nyingine. Hii ina maana kuwa lugha hutofautiana katika michakato ya kimofolojia ya uundaji maneno.

Wataalamu hao walichunguza majina ya mahali na kubainisha mambo mbalimbali ya kiisimujamii yanayosababisha uteuzi wa majina fulani yanayorejelea sehemu mahususi. Aidha, baadhi ya watafiti walizingatia mkabala wa kimofolojia katika kushughulikia taaluma ya onomastiki. Waliangazia vipengele kama vile kubainisha maumbo ya majina ya mahali (Mjapelo, 2009). Walibainisha pia namna majina ya mahali yanavyonyambuliwa ili kuunda majina ya watu waishio katika eneo husika. Buberwa, (2011) alionyesha uamilifu wa viambishi ngeli katika majina ya mahali. Kihore na wenzake, (2004) na Mwendamseke, (2011) walitafiti kuhusu vipengele vya kimofolojia vya nomino za Kibantu kwa kujikita zaidi katika nomino za kawaida pasipo kugusia nomino za pekee zinazotaja mahali. Wataalamu hawa walidai kuwa nomino za mahali huundwa kwa mizizi tu na haziwezi kuchanganuliwa kimofolojia, madai yaliyoungwa mkono na Karanja, P. na Habwe, J. (2007) walioshikilia kuwa nomino za pekee kama vile za mahali hujidhihirisha katika maumbo yake maalum.

Ingawa wataalamu wa awali wamechunguza maana na mbinu za kuunda majina ya mahali, hakuna utafiti uliofanywa kuhusu miundo ya toponemia katika jamii za Wamwimbi na Wamuthambi. Hali hii imesababisha kutofahamika kwa maana na miundo ya toponemia katika jamii hizi. Kuambatana na madai haya ilikuwa muhimu kuchunguza namna toponemia za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi zilivyoundwa. Aidha, utafiti huu ulilenga kuchunguza iwapo toponemia zingeweza kuchanganuliwa kimofolojia.

## MWAUO WA MAANDISHI

**Utafiti Uliofanywa Kuhusu Majina ya Mahali**

Utafiti kuhusu majina ya mahali ulifanywa na Rugemalira (2005) aliyechunguza mofolojia ya majina ya mahali katika jamii ya Runyambo. Matokeo ya utafiti huo yalibaini kwamba majina katika jamii hiyo yaliundwa kwa kutumia utaratibu maalum wa kimofolojia. Hata hivyo, utafiti wa Rugemalira ulijikita katika kuchunguza mofolojia ya majina ya mahali lakini utafiti uliofanywa ulipiga hatua zaidi kwa kuchunguza maana ya toponemia na michakato mingine ya utoaji wa toponemia za shule za msingi za eneo la Mwimbi na Muthambi.

Azhari (2006), alibainisha kategoria ya majina katika lugha ya Kiarabu na kufasili jina kuwa ni kila neno linalotaja mtu, mnyama, mmea, au vitu . Alibainisha aina mbili za majina katika lugha ya Kiarabu ambazo ni majina ya pekee na majina ya kawaida. Alitaja majina maalum kama majina ya mito, miti, maziwa na kadhalika. Maelezo haya yalihusiana na utafiti huu kwa vile, yalifafanua kategoria za majina maalum yakiwemo majina ya mito, mimea, na majina ya vitu ambayo ni kategoria ya nomino maalum sawa na toponemia ambazo zilishughulikiwa katika utafiti huu. Aidha, Azhari (keshatajwa) hakufafanua kwa kina semantiki ya majina hayo wala kuonyesha namna yalivyoundwa suala ambalo lilishughulikiwa katika utafiti huu.

Cameron (1961), alifafanua utoaji wa majina ya mahali katika jamii ya Waingereza. Alibainisha aina mbili za majina ya mahali. Aina ya kwanza ilikuwa ni majina yaliyohusu sura ya nchi ya eneo hilo na ya pili ni majina ya makaazi. Mfano "Greenhill " alieleza kwamba jina hilo lilimaanisha eneo lenye kilima chenye rangi ya kijani. Utafiti wa Cameroon (keshatajwa) ulimsaidia mtafiti katika mada yake kwani aliweza kugundua majina ya mahali yaliyotafitiwa zamani katika jamii tofauti. Kazi ya Cameroon ilitofautiana na kazi hii kwani mtafiti alijikita zaidi katika kuchanganua miundo ya toponemia za shule za msingi za Mwmbi na Muthambi.

Moza (2017) alichunguza michakato na mbinu zilizotumika katika uundaji wa majina ya mitaa katika wilaya ya Unguja. Alidhihirisha vigezo vilivyotumiwa kutoa majina ya mitaa kama vile vya kimaumbile, kijamii na vya kiuchumi. Aidha, alionyesha kuwa mchakato wa uambishaji ulitumika ambao ulichangia kuleta misamiati mipya hasa ya maneno mwambatano katika lugha ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yalimfaidi mtafiti kwa vile alichunguza miundo ya toponemia za jamii na kugundua kuwa ziliundwa kwa kupitia michakato mbalimbali ya uambishaji.

Kulingana na Fatma (2018) majina ya watu mashuhuri yalichangia kuibua majina ya mitaa kisiwani Pemba. Utafiti huu uligundua kuwa majina ya watu mashuhuri yalitokana na mambo mbalimbali kama utawala au kazi walizofanya. Aligundua pia majina ya mitaa kisiwani Pemba yalitokana na majina ya watu mashuhuri. Ingawa utafiti huu ulichunguza namna majina ya watu mashuhuri yalivyochangia utoaji wa majina ya mitaa, ulifaidi utafiti uliofanywa kwa

kuchunguza miundo ya toponemia za shule za msingi katika jamii ya Wamwimbi na Wamuthambi.

Kwa mujibu wa Kirui (2016) majina ya mahali ya Wakipsigisi huundwa kwa kuzingatia mchakato wa uambishaji awali, kati na tamati. Kirui (keshatajwa) alichunguza mofosemantiki ya toponimi katika lahaja ya Wakipsigisi wa eneo la Bomet nchini Kenya. Utafiti huu ulimfaa mtafiti katika kuchunguza michakato ya kimofolojia iliyotumika katika uundaji wa toponemia za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi.

Anindo (2017) alitafiti kuhusu mofosemantiki ya toponemia katika lugha ya Lulogooli katika eneo bunge la Sabatia nchini Kenya. Alichunguza maana za toponemia zinazotokana na uambishaji wa maneno. Alidhihirisha kuwa maana za viambishi vya majina huchangia pakubwa katika utoaji wa maana za toponemia za Lulogooli. Utafiti huu ulikuwa muhimu katika kueleza maana za toponemia na kategoria zake. Maelezo ya Anindo (keshatajwa) yaliwiana na utafiti huu kwa vile ulichunguza maana na miundo ya toponemia za jamii katika eneo la Mwimbi na Muthambi.

## MSINGI WA NADHARIA

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Ujinaishaji kwa mujibu wa Stuart na Gottlob (2001). Mihimili ya nadharia hii ilimsaidia mtafiti katika kuchanganua data ya utafiti. Kwa mfano, mhimili wa mantiki ulimsaidia mtafiti kugundua mantiki iliyohusu michakato ya kimofolojia iliyotumika kuunda toponemia katika jamii. Kwa upande mwingine, mhimili wa ukweli ulimfaa mtafiti katika kubainisha maana ya viambishi vilivyotumika kuunda toponemia katika jamii.

Aidha, mhimili wa ufahamu kamilifu wa kitu au mtu ulikuwa muhimu kwa mtafiti kwani ilimbidi atafute wazee wenye ufahamu wa namna toponemia zilivyoundwa kwa sababu si wote waliweza kuzieleza. Katika mahojiano na wazee wakati mwingine mtafiti alielekezwa mahali ambapo angewapata wazee wenye ufahamu kamilifu wa toponemia na wengine waliachwa kwa kuwa hawakuwa na habari ya kutegemewa. Kwa hivyo, nadharia hii ilikuwa mhimili na dira ya kumulika matendo ya kijamii yaliyoakisi utoaji wa toponemia za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi.

## MBINU YA UTAFITI

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo katika kuchanganua data na kuwasilisha matokeo ya ya utafiti. Mtafiti aliteua sampuli kulingana na sifa za kuwa na uwezo wa kutoa data sahihi kulingana na lengo la utafiti huu. Mtafiti alitumia mbinu ya kimaksudi iliyompa uhuru wa kuteua sampuli zilizo na data iliyohitajika Mugenda na Mugenda (1999). Watafitiwa 50 walichaguliwa: machifu 5 katoka kata 5 za eneo la Mwimbi na Muthambi, manaibu wa chifu 25 kutoka katika kata ndogo 25 za eneo hili. Sampuli hii ilichaguliwa kwa madhanio kwamba ni wenyeji wa maeneo husika na wangekuwa na ufahamu kuhusu majina ya shule zilizo katika maeneo yao ya utawala. Kwa wale ambao hawakuwa na ufahamu huo ilikuwa nafasi nzuri kwao kuuliza kutokana na wenyeji wa kata zao na hivyo walifanikisha utafiti huu. Mtafiti aliteua sampuli ya wazee 20 wenye umri wa miaka 70 na zaidi kwa kutumia mbinu ya kimtandao. Umri huu ulitiliwa maanani kwa kuwa iliaminika kwamba wazee wana maarifa na tajriba ya kutosha kuhusu maana na michakato ya uundaji wa toponemia za Wamwimbi. Data katika utafiti huu ilikusanywa kwa njia ya hojaji na mahojiano. Mtafiti alitumia mbinu hizi mchanganyiko kwa lengo la kupata matokeo yaliyo bora kama walivyobainisha Best na Khan (1998) kwamba mbinu moja haitoshelezi katika kupata data zilizoaminika na kukubalika katika utafiti.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Udondoshaji na Uambishaji awali

Huu ni mchakato wa kuondoa kiambishi awali cha asili katika neno au mzizi wa neno na badala yake kupachika kiambishi kingine tofauti ili kuzua maana mpya. Mchakato wa uambishaji na unyambuaji huonyesha upatanisho wa kisarufi wa vipashio vingine vya sentensi (Rubanza 1996).

Muundo wa jina *Kieni*. Jina hili la shule ya msingi limeundwa kupitia mchakato wa ukaakaishaji. Jina hili lingetamkwa Kyeni ambapo fonimu /y/ ambayo ni ya kaakaa gumu inaondolewa na badala yake irabu/i/ya juu mbele hutumika. Kwa vile Wamwimbi hawana muundo wa sauti mwambatano wa konsonanti mbili au zaidi, fonimu /y/ haitumiki na badala yake irabu/i/ hutumika katika kuunda jina *Kieni*. Kulingana na utafiti huu hii ndiyo toponemia ya pekee iliyozingatia mchakato huu wa uundaji wa maneno katika eneo la Mwimbi.

Jina la shule ya msingi ya *Kajiunduthi* limeundwa kwa kuambisha viambishi awali katika nomino *Nduthi* kama, *Ka+ji+o+nduthi*. Kiambishi -ka huleta dhana ya mahali na -o- ni cha kurejelea nomino inayomilikishwa. Nomino *nduthi* ndio mzizi ulio na maana ya kifaa kilichotumiwa katika ufuaji vyuma. Kwa hivyo jina Kajiunduthi limetokana na uambishaji awali. Kuna mabadiliko ya irabu /o/ kuwa /u/ katika maandishi ya jina hili. Kwa hivyo, badala ya kuandikwa kama *Kajionduthi* likawa *Kajiunduthi* kupitia mchakato wa mpishano huru (Karanja na Habwe, 2004).

Jina *Kajiethetu* limeundwa kwa kuzingatia mchakato wa uambishaji awali kama *Ka+ji+i +ithitu* → *Kajiithitu* lenye maana ya uwanja. Kiambishi ka- kina dhana ya mahali, kiambishi -ji- kina maana ya kumilikisha na kiambishi /i/ kina dhana ya ukubwa wa nomino. Jina hili lina maana kuwa mahali penye uwanja. Kunatokea uwiano wa irabu ambapo irabu /i/ zinafuatana na kufanya matamshi kuwa magumu. Kwa sababu hii irabu /i/ moja inabadilika na kuwa irabu /e/.

Kwa hivyo, jina hili linatamkwa *Kajiethetu* kwa mfano, *Ka+ji+e+ithitu→Kajiethitu.*

Asili ya muundo wa jina la shule ya msingi ya *Chogoria* ni kitenzi jina *kunyogoria* chenye maana ya kuharibu. Mzizi wa kitenzi hiki ni -*nyogor*- unaoambishwa ku- ya kitenzi jina, -i- na -a- vya mnyambuliko kwa mfano, *ku+nyogor+i+a.* Katika kuunda jina Chogoria kiambishi –ny- ambacho ni sehemu mojawapo ya mzizi na vilevile kitamkwa cha nazali ya kaakaa gumu. Kiambishi –*ny*- kinadondoshwa kwa vile ingekuwa vigumu kutamka vitamkwa *[ch]* na *[ny]* pamoja katika neno moja. Kwa mfano, *cho+gor+i+a* limetokana na mabadiliko ya kitenzi *kunyogoria* ambacho muundo wake ni *Ku+nyogor+i+a.* jina Chogoria linatumika leo kurejelea eneo kubwa linalojumuisha lokisheni nzima katika sehemu ya Mwimbi Magharibi.

Jina *Kimuchia* limeundwa kutokana na mzizi wa kutenzi jina *kubuchia* chenye maana ya kutupiliwa mbali. Mzizi wa kitenzi ni –*buch*- unaoongezwa viambishi –i- na –a- vya utendaji. Mchakato wa kudondosha kiambishi ku- na upachikaji wa kiambishi ki- unafanyika ili kufanya kitenzi kuwa nomino. Mfanyiko mwingine unaotokea ni kudondosha fonimu /b/ ya mzizi wa kitenzi na badala yake fonimu /m/ inapachikwa kwa mfano, ku+buch+i+a huwa → ki+much+i+a→Kimuchia

Jina la shule ya msingi ya *Kiera* limeundwa kutokana na nomino ya kawaida *Ira* ambayo katika lahaja ya Kimwimbi humaanisha chokaa. Nomino hii imeambishwa ki- ya umilikishi katika ngeli ya KI-VI ili kuunda jina Kiera. Kwa vile si rahisi kutamka /i/ ikifuatwa na /i/ (Bakari 1983), hii ndiyo sababu vokali /i/ zinaungana na kuwa /e/ katika jina Kiera. Huu ni mchakato wa kuungana kwa irabu katika mazingira ya irabu nyingine, Ki+i+ira→ Kiera.

Jina la shule ya msingi ya *Wiru* limeundwa kutokana na udondoshaji wa viambishi -u- na -k- katika neno *ukeru* ambalo lina maana ya umaskini wa kupindukia. Viambishi hivyo vikidondoshwa nafasi yavyo inachukuliwa na nusu vokali /w/ halafu panatokea uwiano wa irabu ambapo vokali /e/ inabadilishwa na vokali /i/. Kwa hivyo jina Wiru linatokea likiwa na sura mpya lakini asili yake ni *Ukeru* ambayo ni nomino dhahania yenye maana ya umaskini wa kupindukia.

Jina *Mwimbi* limeundwa kwa kuzingatia mchakato wa vokali kuwa nusu vokali. Hili ni badiliko linalokumba vokali za Kiswahili ambapo vokali hubadilika kuwa nusu vokali. Vokali ambazo hukumbwa na badiliko hili huwa ni /u/ na /i/. Vokali hizi zinapofuatwa na vokali ambazo ni tofauti nazo huwa nusu vokali. Sheria zinazohusika ni /u/>/w/ v (isiyo /u/). Hii ina maana kuwa vokali ambazo ni tofauti nazo huwa nusu vokali. Katika mfano huu, vokali /u/ hubadilika kuwa nusu vokali /w/ katika mazingira ya kutangulia vokali isiyo /u/ yenyewe. Kwa mfano, muana -*mu vokali* /u/ hubadilika kuwa nusu vokali /w/ katika mazingira ya kutangulia vokali isiyo /u/ yenyewe kwa mfano, muana mu+ana→mwana. Kwa kuzingatia sheria hii, jina Mwimbi limeundwa hivi: mu+imbi→Mwimbi. Mchakato huu vile vile umetumiwa kuunda jina Mwimbi kutokana na kitenzi *kuiumba* ambacho asili yake ni *kujiiumba* chenye maana ya kujiweza. Ku+i+umba →kuĭumba. Kwa kufuata sheria hii kitenzi *kuĭumba* hutumika kuunda jina la mtu anayejiweza (*Muiumbi)* kama ifuatavyo mu+i+u+mba→*mwiumba* ambapo irabu/a/ ya tamati hubadilika na kuwa /i/ katika mpishano huru wa irabu.

**Uambishaji Ka- au ga- Kwenye Mzizi wa Nomino**

Kiambishi ka- hutumiwa kutangulia nomino au mzizi wa nomino ili kuunda baadhi ya toponemia za shule za msingi za Mwimbi. Kiambishi *ka*-au ga- huleta dhana ya udogo wa kitu au umilikisho wa mahali. Baadhi ya toponemia za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi hufuata muundo huu wa uundaji wa toponemia.

Kulingana na wahojiwa wa nyanjani MhG 1 na MhG 8, Jina la shule ya msingi ya *Kathwana* liliundwa kutokana na kuunganishwa kwa Kiambish ka- cha umilikisho wa mahali na mzizi wa nomino '-*Thwana*?. Mzizi huu uliongezwa nazali /n/ kuunda *nthwana* ambazo ni mbegu za miti iliyoitwa Mithwana. Mchakato wa udondoshaji unatumiwa ambapo nazali (n) hudondoshwa na mahali pake pakapachikwa kiambishi Mu- ili kuunda nomino *Muthwana* ambalo ni jina la mti unaozaa *nthwana.* Mzizi -*nthwana* hauna maana bila kuambishwa ka- ya umilikishaji katika kuunda jina Kathwana lenye maana ya Mahali pa *nthwana.* Muundo uu huu ndio hujitokeza *Ka+thwana→Kathwana.*

Jina *Kajiongo* ambalo ni la shule ya msingi iliyo katika eneo la Muthambi limeundwa kwa kuambisha kiambishi ka- mwanzoni mwa jina –*jiongo* linalomaanisha vichwa vingi kwa mfano; *ka+jiongo → Kajiongo.* Kiambishi ka- kinatumika kuonyesha kuwa mahali hapo palikuwa na vichwa ambavyo huitwa *kiongo* katika umoja na *jiongo* katika wingi. Inamaanisha kuwa kulikuwa na mafuvu ya vichwa vingi mahali hapo. Asili ya jina hili ni Kimwimbi kwa kuwa ndio huwa na matamshi ya -ji- ambacho ni kiambishi cha umilikisho wa kitu.

Jina la shule ya msingi ya *Kagongo Gacheke* limeundwa kutokana na jina *Rugongo* ambalo kwa Kimwimbi humaanisha sehemu iliyo ng'ambo ya mto, mlima, ziwa au bahari. Katika kuunda jina hili kiambishi ru- kimedondoshwa kutoka jina Rugongo na badala yake kiambishi ka- kikapachikwa. Matumizi ya kiambishi ka- katika lahaja ya Kimwimbi na Kimuthambi ni kuleta dhana ya udogo. Kwa hivyo mahali au sehemu inayorejelewa ni ndogo. Mchakato

wa kuambatanisha nomino na kivumishi umetumiwa katika kuunda jina Kagongo Gacheke. Gacheke ni kivumishi cha sifa kinachotokana na kivumishi cha dhahania *ucheke* chenye maana ya wembamba. Jina *Gacheke* limeundwa kwa kudondoa kiambishi U- katika kivumishi *ucheke* na kubandika kiambishi Ga- cha udogo wa nomino. Katika lahaja ya Kimwimbi viambishi Ka- na Ga- hutumiwa kuleta dhana ya udogo wa nomino na vivumishi au hali ya kudhalilisha mtu au kitu.

Kathangawe ni jina la shule ya msingi lililoundwa kwa kuzingatia mchakato wa udondoshaji wa irabu /i/ katika jina *Ithangawe* na uambishaji wa kiambishi Ka-mahali pa irabu /i/. Kiambishi ka- huleta dhana ya udogo katika lahaja ya Kimwimbi na Kimuthambi. Matumizi ya kiambishi ka- katika jina hili ni kuleta dhana ya umilikisho wa mahali palipo na wingi wa mawe yaitwayo *mathangawe.*

Kanini ni jina la shule ya msingi ambalo hutumiwa kurejelea kitu kidogo. Huundwa kutokana na kiambishi ka- cha udogo au udunishaji kinapoambishwa kwenye mizizi -nini kutegemea ngeli ya jina linalohusika. Ka +nini→ Kanini. Katika lahaja ya Kimwimbi viambishi vya udogo ni ka- au ga- ambavyo huambishwa kwenye nomino vinapoandikwa au kutamkwa ili kuonyesha udogo wa kitu. Kabla ya kuambishwa kiambishi cha udogo kwa mfano, katika jina *gikombe* (kikombe) kiambishi -gi- hudondoshwa na mahali pake pakachukuliwa na kiambishi ga- (gakombe) hali ya udogo. Katika nomino nyingine kiambishi ka- au ga- huambishwa moja kwa moja katika nomino ili kuifanya kuwa katika hali ya udogo. Kwa hivyo jina *Kanini* liliundwa kutokana na mchakato huu wa kufanya nomino kuwa katika hali ya udogo kama ka + nini→Kanini.

**Udondoshaji na Uambishaji Tamati**

Huu ni mchakato wa kuunda toponemia kwa kudondoa kiambishi awali katika nomino au mzizi wa neno na kujaza pengo linalobaki kwa kiambishi tamati ili kuunda nomino ya mahali.Toponemia nyingi za shule za msingi za eneo la Mwimbi na Muthambi hufuata muundo huu kwa mfano, kiambishi ni- hutumiwa mwishoni mwa nomino ili kuifanya kuwa kielezi cha mahali.

Jina *Kiurani* limeundwa kutokana na uambishaji wa kiambishi Ki- katika nomino *Muura*. *Muura* ni mti wenye shina nene, nyuzinyuzi na huzaa matunda yaitwayo mabuyu kwa hivyo mti wenyewe huitwa Mbuyu. Jamii nyingine huamini kuwa mashetani huishi mapangoni mwa miti hii. Mchakato uliozingatiwa ni kudondosha kiambishi Mu- cha nomino ya wastani na kupachika Ki- cha dhana ya ukubwa wa nomino. Katika Kiswahili kiambishi Ki- hutumika katika udogo wa nomino lakini katika Kimwimbi huonyesha ukubwa. Kwa hivyo katika lugha ya Kimwimbi, Kiurani humaanisha mtu mkubwa aliyeshujaa katika vita au mti mkubwa ulioitwa *muura.* Katika muktadha huu wa toponemia za shule za msingi za Mwimbi, Kiurani limetokana na uambishaji -ni ya tamati katika jina *muura.*

*Kaare* ni jina la shule ya msingi lililoundwa kutokana na mchakato wa kuingizwa kwa irabu.Uingizaji hapa unarejelea uchopekaji wa sauti moja au zaidi katika neno. Uingizaji huu unaweza kuwa wa kimakusudi au kutokea kibahati katika historia ya fonolojia ya lugha (Karanja na Habwe (2004). Jina hili limezingatia muundo wa mvutano wa irabu ambapo konsonanti hufuatwa na irabu mbili. Katika lugha ya Kiswahili muundo huu unapotokea wakati mwingine mchakato wa kudondoshwa kwa vokali hutokea katika mazingira ambapo kuna uziada. Kwa mfano, wa+alimu → walimu, Pa+ake →pake. Mara nyingi vokali zinazofanana hudondoshwa wakati ambapo zinafuatana. Kwa mintarafu hii jina Kaare lilitokana na historia ya fonolojia ya Kimwimbi.Tangu enzi hizo jina hili limedumisha muundo huu ingawa matamshi yake yamebadilika ambapo watamkaji hudondoa irabu /a/ na kuwa *Kare* kwa mfano, Ka+are →kare.

**Udondoshaji na Uambishaji Awali na Tamati**

Toponemia katika kategoria hii ni zao la uambishaji awali na tamati ambapo neno la asili hudondosha viambishi awali kisha mahali pake pakaambishwa viambishi vipya. Mchakato huu wa uambishaji hutegemea mzizi wa nomino inayohusika. Kuna toponemia za shule za msingi katika jamii ya Wamwimbi na Wamuthambi ambazo hufuata mchakato huu wa uundaji wa toponemia.

Jina la shule ya msingi ya *Mutindwa* limeundwa kutokana na kitenzi *gutinda* chenye maana ya kushinda mahali. Muundo huu umezingatia mchakato wa kudondosha kiambishi awali -gu- cha kitenzi jina na badala yake kupachika kiambishi -mu- cha nomino ya mahali. Kiambishi tamati -a cha kauli ya kutenda kinatanguliwa na kiambishi -w- cha hali ya kutendwa. Mu+tind+w+a →Mutindwa. Mabadiliko haya ya kimofolojia yanaleta dhana ya mahali pa kushinda au mahali ambapo watu walikaa sana wakisubiri kuhudumiwa. Wamwimbi walikuwa na msemo, "*kagwatuika Mutindwa?*" kumaanisha (kwani kumekuwa Mutindwa?) kuonyesha dhana ya mtu kukawia sana mahali fulani. Mchakato mwingine uliotumiwa katika kuunda jina kamilifu la shule hii ya msingi ni kutumia nomino+kivumishi+nomino ambapo jina Mutindwa wa Mbogori lilitumiwa kwa kurejelea eneo hili. Siku hizi jina Mutindwa ndilo hutumika kutajia shule hii kwa kuondoa kivumishi kimilikishi *wa* na nomino *Mbogori.*

Jina *Muthenge* limeundwa kutokana na kitenzi *kuthenga* chenye maana ya kurombeza. Jina la mtu anayerombeza ni Muthengi. Ili kupata jina Muthenge kunafanyika mchakato wa udondoshaji wa kiambishi awali -ku- cha kitenzi jina na irabu /i/ ya tamati katika

nomino *Muthengi*. Mabadiliko mengine yanayotokea ni kupachika kiambishi mu- katika mzizi wa nomino na irabu /e/ mwishoni mwa mzizi huo kama, *Mu + theng+e → Muthenge.*

Jina la shule ya msingi ya *Kiamaogo* limepitia mchakato wa uambishaji na udondoshaji wa irabu. Kiambishi *-ki-* cha mahali na *-a-* cha umilikaji huunganishwa kuunda kiambishi *-kia-* chenye dhana ya umilikishaji wa mahali. Irabu /i/ katika jina Miugu inabadilika na kuwa /a/ ya kati chini ili kuifanya kuleta dhana ya matunda badala ya mimea (*miugu*). Irabu /u/ ya juu nyuma hubadilika na kuwa /o/ ya kati nyuma katika mpishano huru wa irabu. Aidha, fonimu /n/ hudondoshwa ili kuunda jina Kiamaogo kama, Ki+a+maogo →Kiamago.

Jina la shule ya msingi ya *Kieganguru* limeundwa kwa kuzingatia mchakato wa vokali kuwa nusu irabi. Katika mchakato huu vokali /u/ hubadilika kuwa nusu irabu /w/ katika mazingira ya kutangulia vokali isiyo /i/ yenyewe kama vile katika kitenzi *kuigagura* (kustaftahi) ku+igagura →kwigagura. Kieganguru limeundwa kutokana na kitenzi *kwigagura* kwa kuambisha -Ki ya mahali na kupachika fonimu /n/ na kubadilisha irabu /a/ ya mwisho kisha kuchopeka irabu /u/ya tamati kwa mfano, Ki+egangur+u → Kieganguru.

Shule hii iliitwa *Makengi* kutokana na neno *gukenga* linalomaanisha kungaa. Kiambishi -ma kimeambishwa mwanzoni mwa kitenzi *kenga* (ngaa) ili kupata jina Makengi. Neno hili limebadilika kupitia mchakato wa mpishano huru ambapo irabu /a/ inabadilika na kuwa /i/. Kwa sababu ya mpishano huu neno Makenga linakuwa makengi kumaanisha vitu vinavyong'aa. Kiambishi -ma- kinafanya nomino itokanayo na kitenzi hiki kuwa katika ngeli ya YA-YA ambapo kiambishi -ma- huonyesha wingi. Mchakato huu unaonyeshwa hapa chini Ma+kengi →Makengi (vitu vinavyong'aa) /a/< /i/> i. Ma+kenga →Makenga, Ma+ keng +i →Makengi. Kwa hivyo jina Makengi hurejelea vitu ving'aavyo.

**Kiambishi Tamati -ni Kwenye Nomino au Mzizi wa Nomino**

Kiambishi -ni kinapoambishwa katika mwisho wa nomino huleta dhana ya kielezi cha mahali. Huonyesha kuwa kuna vitu au kitu mahali fulani. Kuna majina mengi katika eneo la Mwimbi na Muthambi yanayozingatia muundo huu. Kwa hivyo kiambishi ni- hufanya kazi ya kielezi cha mahali na kimilikishi cha nomino.

Jina la shule ya msingi ya *Kauni* limeundwa kwa kuzingatia mchakato wa uambishaji na udondoshaji wa viambishi awali na tamati. Kiambishi -mu- kimedondoshwa kutoka jina *Muu* na kubaki na mzizi –uu kisha kiambishi Ka- cha udogo kikapachikwa ili kuunda jina *Kauu*. Kiambishi tamati -ni cha kilelezi cha mahali kimepachikwa mwishoni mwa jina *Kauu* kuleta dhana ya mahali penye *Kauu* yaani *Muu* mdogo kama inavyoonyeshwa hapa, ka+uu+ni→Kauuni. Kulingana na matamshi mchakato mwingine wa udondoshaji wa irabu hutokea ambapo irabu /u/ hudondoshwa ili kupata jina Kauni. Kwa hivyo jina asili la shule hii ya msingi ni Kauuni lakini kulingana na usajili wa wizara ya elimu shule hii inaitwa Kauni.

Uundaji wa jina la shule ya msingi ya Uthaini umezingatia mchakato wa uambishaji wa kiambishi -ni- cha mahali katika mwisho wa nomino. *Uthai* ni nomino ya dhahania inayomaanisha hali ya kutokuwa na rutuba na mahali pasipofaa kwa kilimo. Uthai+ni→ Uthaini. Kiambishi -ni cha tamati kinaonyesha mahali ambapo pana *uthai*.

Jina *Ndumbini* limeundwa kwa kuzingatia mchakato wa uambishaji tamati. Kiambishi ni- cha mahali kimeambishwa mwishoni mwa nomino *ndumbi* ili kuunda kielezi cha mahali kama vile, *Ndumbi+ni→Ndumbini*. Jina *ndumbi* lina maana tatu mathalan: aina ya kata iliyonakshiwa kwa manyoya ya kuku au ndege na hutumiwa katika uimbaji, nyumba ya mviringo iliyokuwa na paa lililochongoka mfano wa pea au chondo kilichojazwa masuke ya nafaka na mengine kushindiliwa kandokando ili kuzuia yaliyokuwa ndani yasianguke. Wakaazi wa eneo ambalo shule ya Ndumbini imejengwa walikuwa na utamaduni wa kutumia *ndumbi* katika kuimba nyimbo za kiasili jambo lililosababisha mahali hapo kupewa jina hilo.

Jina la shule ya msingi ya *Kirindini* limeundwa kwa kuunganisha nomino na kiambishi cha kielezi cha mahali -ni kama hivi: kirindi+ni→Kirindini. Jina hili linamaanisha mahali palipo na watu wengi. Wamwimbi huwa na matatizo katika kutamka konsonanti /r/ na badala yake fonimu /l/ hutumiwa kama katika jina Kilindini badala ya Kirindini. Fonimu /r/ na /l/ hutamkiwa kwenye ufizi ambapo /r/ ni ghuna na /l/ ni sighuna.

**Muundo Changamani**

Baadhi ya toponemia za shule za msingi za Mwimbi huundwa kwa maneno mawili au zaidi. Maneno ya kategoria moja au tofauti huambatanishwa ili kuunda neno moja. Maneno yanayoambatanishwa hufuata mfangilio maalum ambao ukivurugwa maana pia huvurugika, Buberwa (2010). Toponemia za shule za msingi za Mwimbi huundwa kwa kuzingatia miundo maalum ifuatayo:

**Kitenzi na Nomino**

Data kuhusu kategoria hii ya toponemia zilitokana na utafiti wa nyanjani ulioshirikisha mahojiano ya wazee na hojaji kwa machifu na manaibu wao wa Mwimbi na Muthambi. Taarifa zilizopatikana zilionyesha kuwa toponemia za shule za msingi za

Mwimbi na Muthambi zilitokana na muundo changamano kama wa kitenzi na nomino.

Jina la shule ya msingi ya *Igwanjau* limeundwa kutokana na maneno mawili ambayo ni kitenzi *igwa* kinachotokana na *kugwa* ambapo mzizi wa kitenzi ni -gw- ulioambishwa kiambishi awali cha kuunda kitenzi jina kisha kiambishi -a- cha tamati ili kukinyambua katika hali ya kufanya. Mchakato uliozingatiwa katika kuunda kitenzi hiki ni kuifanya irabu kuwa nusu irabu. Hili ni badiliko ambalo hukumba vokali za Kiswahili ambapo vokali hubadilika na kuwa nusu irabu/vokali. Vokali /u/ hubadilika kuwa nusu vokali /w/ katika mazingira ya kutanguliza vokali isiyo /u/ yenyewe. Mchakato huu ni kama /u/→/w/ /v (isiyo /u/ kwa mfano, katika neno (mu+ana) →mwana, (mu+enu)→ mwenu, Karanja na Habwe (2004). Vivyo hivyo vokali /u/ katika kitenzi *igua* hubadilika na kuwa /w/ na kutamkwa *igwa*. Kiambishi -I- cha awali hutumika katika kuleta dhana ya mahali panapohusishwa na kitu. Katika muktadha huu *Igwanjau* humaanisha mahali ambapo ndama wameanguka (katika maana ya kijuujuu). Kitenzi Igwa huunganishwa na njau ili kuunda jina moja Igwanjau. Kwa hivyo kigezo kilichotumika hapa ni kuunganisha kitenzi na nomino.

Jina la shule ya msingi ya *Igakiramba* limeundwa kwa kuunganisha maneno mawili ambayo ni kitenzi *Iga* kinachomaanisha mahali pa. Inaonyesha umilikisho wa kitu. Nomino Kiramba ni mti ujulikanao kama *Muramba*. Kiambishi ki- cha awali kinatumika kuweka nomino hiyo katika hali ya ukubwa. Hali hii ni tofauti na lugha ya kiswahili ambapo kiambishi ki- huonyesha udogo wa nomino Karanja na Habwe (keshatajwa). Matumizi ya -ki katika jina *kiramba* ina maana kuwa huu ulikuwa mti mkubwa. Mchakato uliotumiwa katika uundaji wa nomino *Igakiramba* ni kudondoa silabi ya kwanza katika *Muramba* kisha kupachika kiambishi ki- moja kwa moja ili kuonyesha ukubwa wa nomino. Dhana inayotumika hapa ni kuwa mahali ambapo shule ya msingi ya *Igakiramba* ilijengwa palikuwa na mti mkubwa uitwao Muramba.

**Nomino Pekee**

Utafiti huu aidha, ulibainisha kuwa baadhi ya toponemia za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi ziliundwa kwa nomino moja pekee. Nomino hizo zingekuwa za watu, mti, hali au kitu mahsusi kilichopatikana mahali fulani. Majina hayo ya kategoria hii hayakufanyiwa mabadiliko yoyote bali yalichukuliwa mazima mazima na kutumika katika kurejelea mahali fulani.

*Kirumi* ni jina la Kimwimbi lililo na maana zaidi ya moja kama yalivyo baadhi ya majina ya Kiswahili. Dhana ya utawe inatokana na matumizi ya irabu (u) katika silabi ya kati -ru- kwenye jina hili. Sauti /u/ inaweza kutamkwa kama /ῦ/ambapo maana tofauti hujitokeza. Inapotamkwa kama/u/jina Kirumi humaanisha laana lakini ikitamkwa kama /ῦ/ huwa na maana ya kuuma. Kwa hivyo dhana hizi mbili hujitokeza kutegemea matamshi ya sauti hizo mbili. Hii ni kwa sababu lugha ya Kimwimbi huwa na irabu saba kama zilivyo baadhi ya lugha za kibantu ambazo ni tofauti na kiswahili ambacho huwa na irabu tano. Jina Kirumi limeundwa kutokana na uambishaji wa kiambishi awali -ku- katika kitenzi -*ruma* ili kuunda kitenzi jina *kuruma* linalomaanisha kuuma au kula kutegemea matumizi ya irabu (u) au /ῦ/ katika matamshi. Kitenzi *kuuma* katika muktadha huu kina manna zaidi ya moja. Kwa mfano, kuuma kwa meno au kubana na kungwatua kitu kwa meno kama vile kuuma nyama au kitu kingine chochote kinachoweza kuumika. Maana nyingine ni kupata kitu kilichowekwa mahali na kwenda nacho kwa idhini ya mwenyewe au kupata bila idhini ambapo itakuwa ni kuiba. Aidha jina hili lilipewa mtu aliyekuwa na tabia, ya kupata au kuuma kitu kama namna ya kumtania. Ingawa hivyo jina Kirumi lilikuwa la mwanamke aliyeolewa kutoka eneo la Kirumi au aliyeishi katika eneo hilo.

Jina la shule ya msingi ya *Murunga* limetumika jinsi lilivyo bila uambishaji kwa sababu ni la mtu.Tofauti ya jina Murunga (mtu) na Murunga (mahali) ni katika matamshi. Katika kurejelea mahali shadda hutiwa katika silabi ya pili kutoka mwisho kwa mfano, Mu'runga lakini linapomaanisha jina la mtu shadda hutiwa kwenye silabi ya kwanza kama, 'Murunga. Hii ni kwa sababu latokana na kitenzi *kurunga* chenye maana ya kukata. Vitenzi vingi vya Kiswahili pia hufuata muundo wa kutia shadda kwenye silabi ya pili kutoka mwisho Mgullu R, (1999). Katika kutamka *Murunga* ya jina la binadamu shadda huwekwa kwenye silabi ya kwanza kwa mfano; *'Murunga.* mifano hii inaonyesha kuwa Kimwimbi ni mojawapo ya lahaja za lugha ya Kibantu inayokaribiana na lugha ya Kiswahili.

Muundo wa jina la shule ya msingi ya *Rugongo* umetokana na mkao wa mahali. *Rugongo* ni mahali ambapo ni ng'ambo ya mto, bahari, mlima au bonde fulani. Jina hili limetumika pasipo matumizi ya viambishi awali kwa vile ni nomino ya pekee. Utafiti huu umegundua kuwa jina *Rugongo* limetumiwa katika sehemu mbalimbali kuliko na mkao sawa kutokana na uwepo wa mito katika sehemu hizo. Kwa mfano kuna shule ya msingi ya *Kagongo Gacheke* na shule ya Kagongo. Aidha, utafiti huu umegundua kuwa kuna sehemu ambazo huitwa Rugongo licha ya kuwa hakuna shule yoyote mahali hapo.

Jina la shule ya msingi ya *Ikumbo* limechukua muundo wa nomino pekee ambapo maana ya nomino inachukuliwa na kutumiwa kutoa jina la mahali. Kwa mujibu wa MhG 4, jina *Ikumbo* humaanisha mahali palipo tambarare baada ya ukingo wa mto au wa bonde. Kulingana na mhojiwa huyu, kuna matumizi ya jina *Ikumbo* katika sehemu mbalimbali kutegemea mito iliyoko na hali ya ujinaishaji ya watu wa sehemu

husika. Kulingana naye, kunaweza kuwa na Ikumbo la mto Tana, mto Mutonga, mto Maara au mto Tungu.

*Minugu* ni jina la shule ya msingi katika wadi ya Mitheru. Maana ya *minugu* ni wingi wa mnyama aitwaye *Nugu* au Nyani. Kiambishi mi- cha wingi wa nomino kimetumika kuonyesha kuwa ni mahali palipokuwa na *Nugu* wengi.Wanyama hao walipenda kula na kuharibu mimea kama mahindi. Kutokana na wingi wa *nugu* katika sehemu hiyo mahali hapo paliitwa minugu. Kwa hivyo shule ya msingi ilipoanzishwa mahali hapo ikapewa jina Minugu.

**Nomino na Kivumishi**

Nomino ni neno linalotaja mtu, mnyama, kitu, mahali au hali nacho kivumishi ni neno linalofafanua kuhusu nomino au kiwakilishi chake Habwe na Karanja (2007). Katika kategoria hii ya toponemia, majina huundwa kwa kuambatanisha nomino na kivumishi ambayo hutamkwa kama neno moja lakini maana yake hujitokeza wazi.

Mchakato uliotumiwa katika uundaji wa jina la shule ya msingi ya *Ndintune* ni kuunganisha nomino na kivumishi Ndi+ntune →Ndintune. Jina hili likiwa kamilifu lilimaanisha ardhi nyekundu kwa sababu jina *ndi* ni nchi au ardhi na *ntune* ni kivumishi chenye maana ya rangi nyekundu. Mahali ambapo shule hii imejengwa pana udongo mwekundu hivyo, ni thibitisho tosha la asili ya jina la shule hii.

Jina la shule ya msingi ya *Kariakomo* limeundwa kutokana na muungano wa maneno mawili ya nomino na kivumishi, Karia+komo. *Karia* ni udogo wa *Iria* linalomaanisha ziwa na *komo* linalomaanisha bila maji au lililokauka. Mchakato uliotumika kuunda jina hili ni uambishaji wa kiambishi -ka- cha udogo badala ya kiambishi -i- cha wastani. Kwa hivyo badala ya kutumia *Iria* (ziwa) hali ya wastani wakatumia *Karia* (kiziwa) katika hali ya udogo. Uundaji wa kivumishi *komo* umezingatia mchakato wa kuungana kwa irabu /a/ na /u/ katika neno *kaumo* na kuwa *komo.* Vokali za Kiswahili huungana katika mazingira ya vokali nyingine kwa mfano ma+ino-meno au ma+ingi-mengi. Hali hii inatokea katika lahaja ya Kimwimbi ambapo *ka+umo → komo.* Badiliko hili hutokea ili kurahisisha matamshi kama anavyodai Bakari(1992).

**Nomino na Nomino**

Toponemia nyingine za shule za msingi katika kata za Mwimbi na Muthambi ziliundwa kwa kuambatanisha nomino na nomino. Tofauti na mchakato wa kutumia nomino na kivumishi ambapo maneno yote mawili huunganishwa, maneno katika kategoria hii hutenganishwa na yote huanza kwa herufi kubwa kwa vile ni nomino za pekee

*Mutiiguru* ni jina la shule ya msingi iliyo katika kata ya Chogoria katika nyanda za juu kunakokuzwa majani chai. Jina hili limeundwa kutokana na mwambatano wa majina mawili *Muti na Iguru*. *Muti* ni mti kwa Kiswahili na *Iguru* ni juu. Kwa hivyo jina hili lilimaanisha mti uliokuwa juu. Muundo wake ni N+ N (Muti+iguru→ Mutiiguru.)

*Mwiria Potters ni* jina la shule ya msingi lililoundwa kwa kuzingatia mchakato wa uambatishaji wa nomino mbili. Mwiria + potters →Mwiria potters. Mwiria ni nomino ya pekee ambayo ni aina ya mti mgumu wa kiasili. Potters ni jina la Kiingereza linalomaanisha wafinyanzi. Mwiria potters kwa hivyo ni wafinyanzi waliotoka katika eneo la Mwiria.

Jina la shule ya msingi ya Ngeru Elite limeundwa kwa kufuata mchakato wa mwandamano wa nomino. Majina mawili tofauti yametumika pamoja ili kuunda jina la shule hii. Jina Ngeru ni la mahali ambapo shule imejengwa na Elite linamaanisha watu waliosoma. Muundo wake ni Ngeru + Elite→Ngeru Elite.

Jina la shule ya msingi ya *Gate* way limeundwa kwa kutumia majina mawili ya Kiingereza ambayo ni *Gate* linalomaanisha lango na *Way* linalomaanisha pa kupitia Gate+way→Gateway. Matumizi ya jina hili ni kuonyesha kuwa wanafunzi ambao hujiunga na shule hii huwa na uhakika wa kuendelea na masomo katika shule mashuhuri za upili na hatimaye kuingia vyuo vikuu.

**Nomino, Kihusishi na Nomino**

Utafiti huu ulibainisha kuwa kulikuwa na toponemia moja ya shule ya msingi katika maeneo ya Mwimbi na Muthambi iliyoundwa kwa kuzingatia mchakato wa nomino, kihusishi na nomino (N+ H+ N). Aina hizi za maneno zimetumiwa pasipo kuunganishwa kwa hivyo kila moja limeanza kwa herufi kubwa. Jina la shule ya msingi ya *Muthigiri wa Ikorani* limeundwa kwa kuzingatia uambatanishaji wa maneno matatu yenye maana tofauti kiisimu. *Muthigiri* lina maana ya mti uitwao *muthigiri* ambao huwa mkubwa na majani yake huliwa na mbuzi. Kuna kihusishi -wa kinachohusisha nomino Muthigiri na Ikorani. Ni kihusishi cha ngeli ya U-YA katika lahaja ya Kimwimbi. Mchakato uliotumiwa ni N+H+N→N. Katika mchakato huu, nomino pekee (*Muthigiri*) imehusishwa na Ikorani (matatizo) kwa kutumia kihusishi cha -A unganifu (wa) pamoja na nomino Ikorani kama hivi, *Muthigiri + wa + Ikorani→Muthigiri wa Ikorani*

**Udondoshaji wa Kiambishi Awali Pekee**

Mchakato mwingine wa uundaji wa toponemia za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi ni kudondoa kiambishi awali pekee kutoka nomino asilia na kisha kubaki na jina la shule mojawapo. Maneno haya huwa nomino za pekee kwa hivyo haziambishwi tena.

Muundo wa jina *Iriga* umetokana na kitenzi *ntiriga* kinachomaanisha sijawahi. Kiambishi awali *nti-* ambacho ni sawa na kiwakilishi cha nafsi ya kwanza umoja –ndi- chenye dhana ya ukanusho kinadondoshwa. Mzizi *iriga* unabaki ambao hauna maana katika muktadha huo wa matumizi. Muundo huu huonekana hivi:
Nt >iriga→Iriga.

Muundo wa jina la shule ya msingi ya *Ngaita* umetokana na jina la mtu kwa hivyo limeundwa kwa kuzingatia mchakato wa udondoshaji wa kiambishi awali. Jina asili ni Mungaita. Kiambishi Mu- chenye maana ya kubinadamuisha sifa ya '*guita*' lenye maana ya kuua kimedondoshwa ili kubaki na jina Ngaita kama inavyoonyeshwa katika mfano huu Mu > ngaita → Ngaita.

Jina la shule ya msingi ya *Kiini* limeundwa moja kwa moja kutokana na jina la asili la ukoo wa Akiini. Mabadiliko yaliyofanyiwa jina hili ni kudondosha kiambishi awali -A- kinachotambulisha watu na -kiini kinachoonyesha ukoo. Kwa hivyo A>Kiini→ Kiini huonyesha mchakato wa kuondoa kiambishi a- kwenye jina Akiini ili kubaki na jina Kiini ambalo ni toponemia ya shule ya msingi iliyo katika kata ya Mitheru.

**Udondoshaji na Mvutano wa Irabu**

Irabu za Kimwimbi zinaweza kudondoshwa wakati mwingine kama zilivyo za Kiswahili. Udondoshaji huu hutokea katika mazingira ambapo kuna uziada. Mara nyingi irabu zinazofanana hudndoshwa wakati ambapo zimefuatana. Kulingana na utafiti huu kuna toponemia moja tu ya shule ya msingi katika eneo la Mwimbi inayozingatia muundo wa udondoshaji na mvutano wa irabu.

Jina la shule ya msingi ya *Maatha* limetokana na kitenzi *kubathuka* linalomaanisha kutengana. Kitenzi hiki kimeundwa kutokana na nomino *mabatha* yenye maana ya njia panda. Nomino hii imeundwa kwa kuzingatia mchakato wa udondoshaji wa kitamkwa /b/ ili kuacha mvutano wa irabu /a/ katika muundo ufuatao: Ma>b+*atha→Maatha.*Asili ya jina hili kimatamshi ni Kimuthambi (*Mabatha*) lakini matamshi yanayotumika sasa ni ya Kimwimbi (*Maatha*).

**Mabadiliko ya Fonimu ya Mzizi**

Utafiti huu uliweza kubaini toponemia moja tu ya shule za msingi za Mwimbi na Muthambi ambayo huzingatia mchakato wa uundaji wa toponemia kwa kufanya mabadiliko ya fonimu ya mzizi. Mabadiliko haya yalitokana na tofauti ya kimatamshi katika lugha ya Kimwimbi na Kitharaka.

Taarifa kuhusu jina la shule ya msingi ya Nkajari ilipatikana kutokana na MhG 16 na 19, walioeleza kuwa limeundwa kutokana na kitenzi *nkaja* na kiulizi *ri?* Asili ya neno hili ni Kitharaka likiwa na maana ya Nitakuja lini? Watharaka hutumia fonimu /y/ badala ya /j/ katika kitenzi *nkaya* kwa maana ya nitakuja. Kiambishi /ri/ cha tamati kina dhima ya kuuliza swali lini? Kwa hivyo, kiulizi asili ni 'Nkajari'. Inadhihirika kuwa Wamwimbi walibadilisha fonimu /ɟ/ kuwa /j/ lakini wakadumisha irabu /a/ inayotumiwa na Watharaka badala ya fonimu /e/ itumiwayo na Wamwimbi. Katika lahaja ya Kimwimbi jina la shule hii lingekuwa *Nkejari* bali sasa linatamkwa *Nkajari* kutokana na matamshi ya asili ya lafudhi ya Kitharaka.

**HITIMISHO LA UTAFITI**

Utafiti huu ulipambanua miundo ya toponemia za shule za msingi katika jamii za Wamwimbi na Wamuthambi. Mtafiti aliongozwa na lengo mahsusi na swali la utafiti. Matokeo yalionyesha kuwa toponemia katika jamii ziliundwa kwa kuzingatia michakato mbalimbali ya udondoshaji na uambishaji awali na tamati katika nomino.

**ORODHA YA VIFUPISHO**

MhC: Mhojiwa kutoka sehemu ya Chogoria
MhG: Mhojiwa kutoka sehemu ya Ganga
MhK: Mhojiwa kutoka sehemu ya Kiera
MhM: Mhojiwa kutoka sehemu ya Muthambi
C.C.M: Church of Scotland Mission
E.A.P.C: East Africa Pentecost Church
P.C.E.A: Presbyterian Church of East Africa
N: Nomino
V: Vivumishi

## MAREJELEO


- Anindo, C. (2017). A Morphosemantiki study of toponyms: Lu.logooli Place names. Unpublished Masters Thesis, University of Nairobi.
- Azhar, H. (2006). Sharhi Tasrih Ala Tawdhih, Beirut: Dar-el-kutub Al-ilmiyah.
- Bakari, M. (1992). The Morphophonology of Kenyan Swahili Dialects. Tasnifu ya Phd (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Bauer, L. (1983). English Word-Formation. Cambridge; CUP.
- Best, J, & Khan, J. (1998). *Research in Education*, New Jersey, Eaglewood Cliffs.
- Buberwa, A. (2011). *Viambishi ngeli katika nomino za pekee: mifano katika majina ya Kihaya*, Kiswahili, Juz. 74. Kur. 41 – 48
- Cameroon, K (1961) English Place Names. London, Exford University Press
- Habwe, J. & Karanja, P (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.
- Habwe, J., & Karanja, P. (2007). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.
- Halle, M. (1973). Prolegomena to a theory of word formation.Linguistic inquiry, 4(1), 16. Retrieved from Scholar.google.com/scholar?hl=en&q=halle+prolegomena+a+theory

- Haspelmath, M. (2002). Understanding morphology. New York: Arnold.
- Jensen, T., & Jensen, J. (1990). Morphology: word structure in generative grammar (Vol.70). Amsterdam; Philadelphia: J. Benjamins Publishing Company
- Kihore, P., & Wenzake, (2004). *Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu:* Sekondari na Vyuo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.
- Kirui, R. (2016). A morphosemantic study of Kipsigis toponyms. Tasnifu ya MA. (Isiyochapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Majapelo, P. (2009). Namna ngeli zinavyosaidia kuunda majina ya watu (unpublished) M.A Dissertation. University of Dar-es-salaam.
- Matinde, R. (2012). *Dafina ya Lugha. Isimu na Nadharia kwa Sekondari na Vyuo vya Kati na vyuo Vikuu.Mwanza:* Serengeti Educational Publishers (T) ltd Mwanza.
- Mgullu, R.(1999). *Mtalaa wa Isimu. Fonetiki, Fonología, na Mofolojia ya Kiswahili*. Longhorn.
- Moza, O. (2017). Michakato na mbinu zinazotumiwa katika uundaji wa majina ya mitaa katika Wilaya ya mjini Unguja, Tasnifu ya M.A. (Isiyochapichwa) Kikuu Huria, Tanzania.
- Mphande, L. (2006). *Naming and Linguistics Africanism in African- American Culture*. New York: Ohio University.
- Mugenda, M., & Mugenda, G. (1999). *Research Methods: qualitative andquantitativeapproach.* Acts press Nairobi.
- Mwenamseke, F. (2011). Uainishaji wa ngeli katika lugha ya Kibena. Tasnifu ya M.A. (Isiyochapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Plag, I. (2003). Word-formation in English. Cambridge University Press.
- Rubanza, Y. (1996). The Linguistic Creativity of Haya Personal Names.*Journal of Institute of Research*, Vol. 63, TUKI, Dar es Salaam
- Rugemalira, J. (2005). *A Grammar of Runyambo*, Dar es Salaam: Language ofTanzania Project, University of Dar es salaam.
- Stuart, M. na wenzake. (2001). *Different types of dictionaries.* Grin Verlang.
- Wodak, R. (2001). *Methods of Critical Discourse Analysis.* London: Sage publications.


**Cite This Article:** David Micheni Mutegi, Allan Mugambi, Timothy Kinoti M'Ngaruthi (2022). Upambanuzi wa Miundo ya Toponemia katika Jamii: Mfano kutoka Jimbo Dogo la Maara nchini Kenya. *East African Scholars J Edu Humanit Lit*, 5(10), 191-200.